

**HABARI KANDA YA ZIWA**


# Waziri Simbachawene awaonya watumishi kudharau wananchi

**Na Benny Kingson,**  
TABORA

**W**AZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewaonya watumishi wa umma kuacha tabia za kuwadharau wananchi na kuhakikisha wanawapa huduma stahiki bila kujali hali za maisha.

Simbachawene alitoa onyo hilo juzi wakati wa mahafali ya 38 ya Chuo cha Utumishi wa Umma cha Uhazili mkoani hapa.

Simbachawene aliwataka watumishi kutambua kuwa wameajiriwa na wananchi, hivyo jukumu lao kubwa ni kuwatumikia kwa weledi na kuttua matatizo yao kwa wakati.

"Tambueni kuwa utumishi wa umma ni ibada, hivyo hakikisheni utumishi wenu unakuwa bora kupitia huduma mnazozitoa kwa utiifu, upole, uadilifu na usikivu kwa wale mnaowahudumia," alisema.

Kwa upande mwengine, aliagiza watumishi wanaojiriwa kupatiwa mafunzo ya awali na kuwajengea umahiri kabla ya kuanza kazi ili watambue miiko na kurahisisha utoaji wa huduma katika ofisi za umma.

Simbachawene, alisema serikali inatarajia kukifanyia ukarabati chuo hicho ili kiwe katika ubora kwa sababu kinaandaa, kutoa watumishi na kufanya tafiti bora za utawala.

Awali akitoa taarifa ya utendaji kazi chuoni hapo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Ernest Mabonesho, alisema



**"Tambueni  
kuwa utumishi  
wa umma ni  
ibada, hivyo  
hakikisheni  
utumishi wenu  
unakuwa  
bora kupitia  
huduma mn-  
zozitoa kwa  
utiifu, upole,  
uadilifu na  
usikivu kwa  
wale mnaowa-  
hudumia,"  
alisema.**

wameongezeka watumishi 278 kutoka 242 ili kuongeza kasi ya utendaji kazi.

"Tuna upungufu wa kompyuta, vifaa vya uchapaji, miundombinu, majengo ni ya zamani tangu mwaka 1972 chuo kinaanzishwa, madarasa hayakidhi mahitaji pamoja na gharama za uendeshaji kuwa kubwa," alisema na kuongeza kuwa: "Pia tutajitahidi kujenga majengo ya chuo katika mikoa ya Singida, Tanga na Mbeya ili kuacha kuendelea kupanga."

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batrida Burian kwenye mahafali hayo, Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Louis Bura, aliwasihii wahitimu hao kuendeleza weli edi walipata chuoni hapo watakapokuwa ili kuisaidia jamii na Taifa.